**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UCHUMI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWA AFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO

**Mheshimiwa Spika,**

Nianze hotuba hii kwa kumshukuru Mola Mtukufu aliyetujaalia afya njema na kutuwezesha kuendelea na shughuli zetu za msingi katika ujenzi wa Taifa letu. Pongezi za dhati tunazitoa kwako Mheshimiwa Spika pamoja na wasaidizi wako, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza kwa jinsi mnavyoliendesha Baraza hili tukufu kwa busara, hekima na umahiri mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Nichukuwe fursa hii kuthamini juhudi anazochukua Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi za kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar kupitia uimarishaji wa sekta ya fedha nchini kwa kuweka mifumo ya kudhibiti mapato na matumizi ya fedha za umma. Hatua hii ni muhimu katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo tuliyojipangia.

**Mheshimiwa Spika,**

Nielekeze salamu zangu za shukurani kwa Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya Salum na Naibu Waziri Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir (Mrembo) kwa ushirikiano wao mkubwa wanaoipatia Kamati ambao

umepelekea kupatikana ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yetu, Aidha, shukrani za dhati zimuendee, Katibu Mkuu wa Wizara hii Dkt. Juma Malik Akil, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kushirikiana nasi katika kazi zote za Kamati yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kanuni ya 107 (3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2020 ambayo maelekezo yake yanapatikana kwenye Jadweli la kwanza inaipa Kamati yetu jukumu la kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia. Kwa mnasaba huo, Kamati ilikutana na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Fedha na Mipango tarehe 30/08/2022 na kupokea taarifa ya utekelezaji wa maoni na maagizo ya Kamati kwa Wizara hiyo yaliyotokana na Ripoti ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,**

Nichukue fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano ya hali ya juu waliyoyaonesha katika kutekeleza majukumu yetu ya Kamati hususan katika kujadilia taarifa ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Maagizo ya Kamati kwa Afisi ya Rais Fedha na Mipango kuhusu utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yetu. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambulisha Wajumbe hao kama ifuatavyo:

1. Mhe. Sabiha Filfil Thani - Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Soud Nahoda - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Rukia Omar Ramadhan - Mjumbe
4. Mhe. Hassan Hamad Omar - Mjumbe
5. Mhe. Panya Ali Abdalla - Mjumbe
6. Mhe. Ameir Abdalla Ameir - Mjumbe
7. Ndg. Nouman Thabit Nouman - Katibu
8. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu

**Mheshimiwa Spika,**

Jumla ya maagizo 34 yalitolewa na Kamati yangu kwa mwaka 2021/2022 kwa Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Fedha na Mipango. Kiujumla, Kamati imeridhika na maendeleo ya utekelezaji wa Maagizo hayo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu imefarajika na juhudi zinazochukuliwa na TRA katika kuondoa muingiliano wa kodi kwa wafanyabiashara wa Zanzibar baada ya kuarifiwa kwamba study ya kuangalia ufanisi wa makusanyo ya kodi kwa upande wa Zanzibar inaendelea na inatarajiwa kukamilika Disemba 2022. Hatua hii ni muhimu katika kutatua changamoto wa ulipaji mara mbili ambayo inawakabili wafanyabiashara wa Zanzibar na kupelekea kupanda kwa bei za bidhaa nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa vile Zanzibar ni nchi ya visiwa, uchumi wetu unategemea zaidi matumizi bora ya bandari zetu. Kwa masikitiko makubwa, Kamati imepokea changamoto za bandari yetu ya malindi ambazo ni:

- Udogo wa bandari unaopelekea kushindwa kufunga gati zaidi ya meli moja
- Vifaa khafifu vya kupakulia mizigo vinavyopelekea mizigo kupakuliwa kwa muda mrefu
- Uwepo wa meli ndefu zinazozidi uwezo wa bandari yetu kuzihudumia
- Kuna udhaifu katika sekta ya uzalishaji nchini unaopelekea meli zinazoleta mizigo kukosa mzigo wa kuondoka nao (export).

Ili kuondoa changamoto hizo zinazopelekea msongamano wa makontena bandarini, Kamati yetu inaendelea kusisitiza mipango mizuri ya Wizara ya kujenga bandari kavu (ICD) eneo la Mpigaduri itekelezwe haraka iwezekanavyo kwa nia ya kuwapunguzia makali ya bei wananchi, kuongeza makusanyo kupitia shughuli za bandari na kuinua uchumi wetu kwa ujumla wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Wataalamu ni chachu ya maendeleo ya sekta husika na Taifa letu. Katika ripoti yake, Kamati ya Uchumi ilitoa maagizo kadhaa kwa Wizara kupitia ZRB juu ya namna ya kuwaenzi na kulinda afya za wataalamu wa sehemu ya mitambo (ZRB data center). Pamoja na majibu mazuri ya Wizara yanayoonesha hatua za kuwaongezea ujuzi wataalamu hao, Kamati yetu haikupata maelezo yanayojitosheleza juu ya hatua za kulinda afya za wataalamu hao ambao ni vijana wazalendo na ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya Taifa hili.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Uchumi inatoa pongezi za dhati kwa Serikali kupitia Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kwa kuanzisha na kusimamia mradi wa VFMS unaowezesha utoaji wa risiti za kielektroniki kwa biashara zote za Zanzibar. Mradi huu utaongeza mapato ya Serikali kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo nchini. Hata hivyo, Kamati imesikitishwa na baadhi ya wawekezaji wa hoteli kutoingia kwenye mfumo huu na kutumia mifumo mengine inayotumika kwenye mataifa yao jambo ambalo ni kinyume na taratibu zetu.

Hivyo, tunaiomba Wizara iwachukuliye hatua wawekezaji hao ili iwe funzo kwa wawekezaji wengine wenye nia ya kufanya matendeo kama hayo.

Katika majibu ya maagizo ya Kamati ya kuhakikisha Wizara inafanya makusanyo kila panapopaswa kutozwa kodi, Kamati yetu imepata wasiwasi ilipoarifiwa kuwa baadhi ya wakwepa kodi wamekua ni wakwepaji sugu na hawashughuliki na faini wanayopigwa na Serikali. Watu hao hulipa faini hiyo na kuendelea na kosa lile lile jambo ambalo linaifanya Kamati kujiuliza maswali mengi bila ya kupata majibu yake. Hivyo, Kamati inashauri Serikali ipitiye upya viwango vya adhabu vilivyowekwa na kutilia mkazo kwenye suala la utekelezaji wa sheria zilizopo ili kuhakikisha kila mmoja wetu anatekeleza wajibu wake kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu imearifiwa kuwa Serikali inayafanyia kazi maeneo mawili ambayo yanaleta changamoto kwa PBZ kujiendesha kibiashara ambayo ni utaratibu wa manunuzi na ajira za watendaji wake. Tunaipongeza Serikali kwa kutoa mwongozo wa kurahisisha huduma za manunuzi kwa mashirika ili manunuzi yafanywe kwa haraka na ufanisi kwa maslahi ya Benki.

Pamoja na hatua hizo, Kamati yetu inatilia mkazo juu ya suala zima la kuchangamkia fursa za biashara zinazijitokeza zikiwemo zile za kukubalika sokoni kama ilivyojitokeza kwenye tawi la PBZ mtwara. Aidha, Kamati inaitaka Wizara kufanya ziara za mara kwa mara kwenye matawi na vituo vya huduma kwa wateja vya mikoani ili kubaini changamoto mapema na kuzitatua kwa haraka kabla hazijaathiri maendeleo ya benki.

Kadhalika, PBZ inahitaji kufanyiwa mapitio (reform) ya mfumo wake mzima wa uendeshaji na kuajiri watendaji kwa mujibu wa sifa zao. Suala hili litawafanya watendaji hao kutoa huduma bora kwa mujibu wa miongozo ya kazi zao na kupelekea ongezeko la wateja litakaochangia kwenye ukuaji wa benki yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kuhusu kadhia ya FBME, Kamati yetu inaipongeza Serikali kwa hatua inazochukua

katika kuhakikisha haki za waathirika wa kufungwa kwa benki hiyo waliopo nchini zinapatikana. Sambamba na hilo, Kamati imebaini kuwepo kwa mwanya wa kisheria ambao hutumiwa na wajanja kutapeli wananchi fedha zao kwa njia ya mtandao.

Hivyo, Kamati inaiomba Wizara kuendelea na utaratibu wa kutunga sheria ya microfinance na kuwanusuru wananchi na utapeli wa mitandaoni na wa vikundi vya watu wasiokua na nia njema.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu inaipongeza Serikali kwa kuonesha nia ya dhati kuliendesha Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) kwa faida, ambapo Wizara imeanza utekelezaji wa agizo la Kamati la kurekebisha sheria ya bima “Motor vehicle Third Party Risk Decree Cap 136” ambayo imebainika kupitwa na wakati. Hatua hii ni muhimu kwa ustawi wa shirika letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imebaini kuwa Msimamizi mkuu wa shughuli za bima nchini (TIRA) ana mapungufu kadhaa na kutoa maoni kwenye ripoti yake ya mwaka wa fedha 2021/2022. Mapungufu makuu yaliyopo ni Mamlaka kutokuwa na Bodi ya kujiendesha tangu mwaka 2019 wakati bodi yake ilipotenguliwa. Aidha, (TIRA) imekosa Sera ya kuiongoza hadi leo. Kwa vile Mamlaka hii ni chombo cha Muungano, tunaiomba Serikali kufanya mashauriano na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya uondoaji wa changamoto hizi ili chombo hiki kiweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena viongozi na watendaji wa Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Fedha na Mipango kwa juhudi wanazozichukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano wao kwa Kamati hii.
Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa makini wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya Kamati yangu, naomba Kuwasilisha.

Ahsante,

.......................................

Mhe. Sabiha Filfil Thani,
Mwenyekiti,
Kamati ya Uchumi,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar**.